## 3.2 KISWAHILI (102)

## 3.2.1 Kiswahili Paper 1 (102/1)

## 1 Lazima

Wewe ni katibu wa jopokazi lililoteuliwa kuchunguza vyanzo vya ongezeko la visa vya wanafunzi katika eneo la Telekeza kuacha shule kabla ya kukamilisha masomo yao. Andika ripoti ya uchunguzi huo.

- 2 Andika insha kuhusu umuhimu wa tamasha za muziki katika maisha ya vijana.
- 3 Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

Usipoziba ufa utajenga ukuta.

4 Tunga kisa kinachoanza kwa maneno yafuatayo:

Nilimtazama kwa muda. Macho yake yalijaa machozi ya furaha na majonzi...